

Rasilimali mali ya nani?



Jishindie kompyuta
ndani!

Kijitabu hiki kimetaryishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza

Waandishi:

Richard Mabala na Winston Churchill Shauri

Mchoraji:

Daniel Mzena

Wahariri:

Rakesh Rajani, Evarist Kamwaga, Joseph Ngwegwe na
Justice Rutenge

Usanifu:

Winston Churchill Shauri



©Tamasha/Twaweza 2012

Barua: S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania

Simu: +255 719 751 928

+255 787 220 233

Barua pepe: rmabala@yahoo.com

wchachi@yahoo.com

Tovuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakilia na kutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Ndugu wasomaji,

Uwekezaji unaweza kuchangia sana maendeleo iwapo wawekezaji wanaongeza uzalishaji na kuboresha miundombinu ili kuongeza tija na pato la taifa hadi mapato ya kaya, pamoja na kuongeza nafasi za ajira. Umuhimu huo ulisisitizwa tena na Mh. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika salamu zake za mwaka mpya 2012. Alisema:

"Katika mwaka huu tunaoumaliza leo tulitoa kipaumbele cha juu katika kukuza uwekezaji nchini na tunakusudia kuendelea kufanya hivyo mwaka ujao...Lengo letu kuu la kuhimiza uwekezaji nchini ni kutaka kuongeza uwezo na kasi ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa kuongeza uzalishaji mali, kuboresha huduma na kukuza ajira..."

Lakini uwekezaji ukiwanyang'anya wananchi rasilimali yao na uwezo wao wa kuijendeleza bila kuleta faida nyngine kwao, unageuka kuwa kero kwa wananchi hata kama unaongeza pato la taifa kwa ujumla. Mfano mmojawapo ni migogoro iliyopo kwenye maeneo ya migodi mingi, pamoja na mashamba makubwa ya wawekezaji. Matokeo yake ni kwamba wananchi wengi wamehoji mikataba inayosainiwa na wawekezaji wakubwa na wadogo, hasa upande wa migodi lakini pia kwenye maeneo ambapo wananchi wamepoteza ardhi yao au uwezo wao kufikia rasilimali nyngine kama vile maji, misitu, au umeme n.k. Ni muhimu sana wananchi, kwa kushirikiana na serikali na asasi za kiraia, kuhakikisha kwamba uwezekaji unaboresha maisha ya wananchi wa eneo lile, siyo kuyaharibu.

Maji ni rasilimali muhimu sana. Kwa mujibu wa MKUKUTA, zaidi ya nusu ya wananchi wa Tanzania wanapata maji safi na salama karibu kutokana na maji ya bomba, kisima kilicholindwa au chemchem. Lakini huko vijijini, chini ya 40% ya kaya wanapata maji hayo na katika wilaya saba, ni chini ya 10%. Lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba 90% ya watu wanapata maji safi na salama lakini safari bado ni ndefu.

Rasilimali nyingine muhimu sana ni rasilimali watu. Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe ili mradi wanapata fursa kufanya hivyo. Lakini sehemu nyingine inaonekana sasa kwamba tunategemea ufadhili na uwekezaji kufanya kazi badala ya sisi wenyewe.

Kwa mfano, vijana ni 35% ya wananchi wote wa Tanzania lakini kwenye jamii nyingi, wanatumikishwa tu kwenye miradi ya maendeleo kama wafanyakazi wasio na ujira. Sanasana wanapatiwa mikopo yenyeye riba kubwa ili waweze kutafuta kujikimu na biashara ndogondogo.

Hatujatambua hazina kubwa ya uwezo wao. Wakipewa nafasi wanaweza kuendeleza sana jamii zao huku wakijiedeleza wenyewe. Kijitabu hiki kinaonyesha hivi upande wa maji lakini kuna mambo mengi ambao vijana wanaweza kufanya, kwa pesa na motisha kidogo tu. Ndiyo wenyeye nguvu na ubunifu.

Hali ikoje kwetu?

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha

Wahusika



Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo na mkereketwa wa maendeleo

Bonge:



Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Bibiye:



Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mwenyekiti:



Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

Mtendaji:







Baadaye asubuhi





Wanatuonea.
Tunajitahidi kujikimu.
Sasa hata kuchota
maji noma.

Mbona
lilipasuka
lenyewe siku
nyingi ndipo
tulianza bustani
yetu.

Hatukubali!
Twendeni
Ofisini.





OFISI YA KATA

Nyie vijana ni
Wakorofii.
Mmeshatangaziwa
bomba ni la
mwekezaji.

Kwa hiyo?
maji yanavuja,
tusiyatumie?

Tuna
mkataba na
mwekezaji.

Mkataba wa
kutunyima
sisi maji?






Hili liwe
fundisho kwenu.
Maji yana
wenyewe.

Na ole
Wenu mchote
tena.







Usitujibu jeuri hapa.
Maji hatupati. Ujiana
wetu wanakamatwa
bila Sababu.

Kazi yako
Kutunyima maji
mgeni afaidike!

Hapiti mtu
hapa Leo.







Tolieni jamani.
tutafute njia ya
kutatua hili.

Siku zote
mmeekaa kimya
tu wakati tunateseka!

Tunataka
mkutano na
mwekezaji!

Sawa.



Bustanini kwa vijana





Mkutano wa kijiji

Mwekezaji hakuweza kufika.
ila kuna mwakilishi wake.
Tulishajadiliana naye na
huyu atawaeleza.





Bosi wangu amekubali
atakarabati na kuunganisha
bomba kila Kijiji. Lakini
maji yatumike kwa
zamu.

Habidi tuunde
kamati ya maji.

Zamu gani!
Kuchota maji
saa saba
za usiku?

Hebu
tusikilizane
kwanza.







Je wajua?

1. Chanzo cha hiki kitabu ni matokeo ya utafiti uliofanywa na TAMASHA huko Musoma, ambapo vijana walikamatwa kwa kutumia maji ya dimbwi kutokana na kupasuka kwa bomba. Bomba lenyewe liliwekwa mwaka 1972 lakini lilikuwa halikarabatiwi.
2. Kulingana na sheria ya ardhi wananchi wanapaswa kushiriki katika maamuzi kuhusu uuzaaji wa ardhi ya kijiji kwa watu wa nje.
3. Mara nydingi, upatikanaji wa maji safi na salama ni kipaum-bele cha kwanza cha wananchi, hasa wanawake. Ndiyo maana ushiriki wa wananchi katika kamati za maji uko juu (13%) ukilinganisha na ushiriki wao katika kamati zingine. Maji ni uhai.
4. Lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba maji safi na salama hayako mbali zaidi ya mita 400 kutoka kwa kila kaya¹.
5. Ukosefu wa ajira humaanisha kwamba rasilimali watu haitumiki ipasavyo. Kwa mujibu wa MKUKUTA, 15.4% ya vijana wa kike na 14.3% ya vijana wa kiume hawana ajira. Lakini bila shaka asilimia ni kubwa sana maana kuna vijana wengi wanaobangaizabangaiza bila kuwa na kazi maalum.
6. Ingawa wengine huona kwamba mikopo ni ukombozi kwa vijana, utafiti wa TAMASHA ulionyesha kwamba vijana wengi wanaogopa kuchukua mikopo kwa sababu ya ukali wa riba isiyozingatia hali yao. Walisema kwamba wanaogopa kupoteza hata kile kidogo walicho nacho.

¹ MKUKUTA 2010



Tufanye nini?

1. Wananchi tukiwa macho kuanzia mwanzo wa kuingia kwa mwekezaji, tunaweza kuhakikisha kwamba mkataba unaosainiwa na kijiji au ngazi za juu zaidi, ni kwa manufaa ya wote.
2. Katika kufuatilia bajeti ya kijiji, itakuwa rahisi kujuua kodi zinazolipwa na mwekezaji na kama anazilipa kweli.
3. Wakati vijana wengi wanajitegemea na wanatafuta kujikimu, ni muhimu kutambua na kulipia kazi zao katika jamii badala ya kutegemea waache shughuli zao za kukijimu kwa kulazimishwa tu. Wakilipiwa angalao posho, hata huduma ile itakuwa bora zaidi.
4. Vijana wanaweza kufanya kazi nyingi nyingine za jamii kama vile ufuatiliaji wa afya ya watoto, elimu ya watu wazima, utafiti wa eneo, ulinzi wa mazingira, elimu rika, n.k.

Shindano

Toa maoni, jishindie kompyuta!

Ndugu msomaji, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imeahidi kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kupitia mpango huu, Serikali inataka kukusikia.

Toa maoni yako kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii; maji, elimu na afya.

Tuambie wazo moja kuboresha elimu, afya au maji. Halafu, tuambie mwananchi afanye nini kuleta mabadiliko.

Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2013, maoni kumi bora yatachaguliwa na kila shule itakayotoa washindi itapatiwa kompyuta ndogo mbili (laptops). Pia, maoni ya washindi yatachapishwa kwenye vitabu na tovuti.

Sharti: Kila mtu anaweza kutuma maoni, lakini zawadi zitatolewa kwa watakaondika *kupitia* shule zao tu.

Tuma maoni yako kabla ya tarehe 1 Novemba, 2013

Anuanı: OGP Tanzania, S.L.P 38342, Dar es Salaam

Barua pepe: unaselmaje@gmail.com

Kumbuka kuweka taarifa hizi:

- Tarehe
- Majina kamili, umri wako, jina la shule; jinsia (me/ke)
- Anuani kamili: SLP na makazi (kata, wilaya na mkoa); namba ya simu; barua pepe

Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership - OGP).

Open
Government
Partnership



Mpango wa OGP unahimiza shughuli za Serikali ziendeshwe kwa uwazi zaidi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, mwitikio wa Serikali, kupambana na rushwa na kujenga kuaminika zaidi. Twaweza inashirikiana na Serikali kuendeleza uwazi na ushiriki wa wananchi kupitia Mpango wa OGP.